

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE
NA MAKUNDI MAALUM



TAARIFA KWA UMMA

UCHAGUZI MKUU WA BARAZA LA TAIFA LA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kikao chake cha 52 kilichoketi tarehe 14 Machi, 2024 Jijini Dodoma, pamoja na mambo mengine, imeridhia kuanza kwa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unaotarajiwa kufanyika kuanzia mwezi Aprili 2024 hadi Juni 2024 baada ya uongozi uliopo sasa kuelekea kumaliza muda wake ifikapo tarehe 30 Juni, 2024.


Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali limeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 25(1) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 5(b)(ii), 5(c)(v) na 5(f)(iv) ya Kanuni za Uchaguzi za Baraza za mwaka 2016, Uchaguzi wa Viongozi wa Kitaifa wa Baraza, Wenyeviti wa Kamati Ndogo na Wajumbe wa Bodi, utafanyika kila baada ya miaka mitatu.

Itakumbukwa kuwa, Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza katika ngazi ya Wilaya ulifanyika tarehe 26 Juni, 2021; katika ngazi ya Mikoa ulifanyika kati ya tarehe 28 Juni, 2021 na tarehe 02 Julai, 2021; na kwa upande wa Wawakilishi wa Makundi Maalum (Mashirika ya Kimataifa, Mashirika ya Watoto, Mashirika ya Vijana na Mashirika ya Watu Wenye Ulemavu) ulifanyika tarehe 05 Julai, 2021.

Vilevile, Uchaguzi wa Viongozi wa Kitaifa wa Baraza (Mwenyekiti, Katibu Mkuu na Mweka Hazina); Wenyeviti wa Kamati Ndogo (Kamati ya Fedha na Utawala Kamati ya Kujengea Uwezo; Kamati ya Maadili; na Kamati ya Mawasiliano na Utandaa); pamoja na Wajumbe wa Bodi ulifanyika tarehe 08 Julai, 2021 Jijini Dodoma.

Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inawaalika wanachama na wafanyakazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wa Baraza kuanzia katika ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Aidha, Bodi inatumia nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Baraza wanaomaliza muda wake kwa utumishi wao mahiri kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Tarehe ya kuanza rasmi kwa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pamoja na kutolewa kwa Mwongozo wa Uratibu wa Uchaguzi huo utatangazwa katika siku zijazo na Kamati ya Uchaguzi wa Baraza.



Hajjat Mwantumu B. Mahiza
Mwenyekiti

BODI YA URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

15 Machi, 2024